



Mahitaji ya Chanjo Kujiandikisha katika Gredi ya 7 ya 2021-2022

Ili kuhudhuria gredi ya 7, lazima *mwanafunzi awe na uthibitisho ulioandikwa* wa kupokea chanjo zifuatazo:

- ◆ **Tdap**
- ◆ **2 Ukambi, Matumbwitumbwi, Rubela (MMR)**
- ◆ **3 Ugonjwa wa ini (Hepatitis B)**
- ◆ **2 Varicella (tetekuwanga)**
- ◆ **1 Meningococcal** (*Chanjo ya Meningococcal Conjugate pekee inayotolewa baada ya umri wa miaka 10 ndio inayokubalika kwa uandikishaji shuleni katika gredi ya 7.*)
- ◆ **4 Polio**
- ◆ **2 Ugonjwa wa ini (Hepatitis A)**
- ◆ **5 DTaP/DT**

Imependekezwa kwa watoto wenye miaka 11-12 lakini haihitajiki kwa ajili ya kujiandikisha shule huko Utah:

- ◆ **HPV**
- ◆ **Mafua**
- ◆ Chanjo ya **COVID-19** inapendekezwa kwa watoto wenye **umri wa miaka 12** na zaidi

Uthibitisho wa kinga dhidi ya magonjwa unaweza kukubaliwa badala ya chanjo iwapo tu hati kutoka kwa mhadumu wa afya inayosema kwamba mwanafunzi aliambukizwa ugonjwa huo hapo awali itawasilishwa shuleni.

Kwa watoto ambao wazazi wao wanadai wasipewe chanjo kwa sababu za matibabu, kidini au kibinafsi, lazima mtu anayewajibika kisheria akamilishe moduli ya elimu ya chanjo mtandaoni katika immunize.utah.gov au kushauriana ana kwa ana katika idara ya afya ya eneo lako. Lazima nakala ya cheti iwasilishwe kwa shule au afisa wa ulezi wa watoto.

Kwa ruhusa ya kutopokea chanjo zinazohitajika, lazima fomu iliyojazwa ya kutopokea chanjo na taarifa iliyoandikwa iliyotiwa saini na mtoa huduma wa afya aliyeidhinishwa iwasilishwe shuleni.

Kwa maswali kuhusu hali ya chanjo ya mtoto wako, wasiliana na mtoa huduma wa afya ya mtoto wako, idara ya afya ya yako eneo lako au Nambari ya Dharura ya Chanjo katika 1-800-275-0659.

Hii inaweza kunakiliwa na kusambazwa.
Ilirekebisha 07/2021